PARLIAMENT
OF KENYA
LIBRARY

# TAARIFA FUPI YA MAENDELEO MATUGA

## UKOMBOZI NA MANUFAA YAKE

MTAYARISHAJI:

SULLEMAN MWARONGA KAMOLLEH
MBUNGE WA ENEO LA MATUGA

TOLEO LA TATU MWAKA 2001

# SEHEMU YA KWANZA (I)

## 1.0 UKOMBOZI WA MATUGA UMELETA NINI?

Tangu eneo la Matuga likombolewe kutoka kwa madharau, minyanyaso, wizi na mengi ya ukoloni mamboleo hapo mwaka wa 1997, tumeweza kuibuka na bahati ya faraji, usaidizi na hata pia kujua mengi ambayo hayakuwepo hapo zamani. Ni mengi yaliyogeuka na mengi pia tuliyopata tangu ukombozi huo. Hapa chini tutafafanua kiasi haba tu ya mafanikio hayo.

### 1.1 KUONGEZEKA KWA JUHUDI ZA PAMOJA

Mwaka huu wa 2001, watu wa eneo la ubunge la Matuga wamezidisha bidii zao maradufu. Tofauti zao za kisiasa na kidini zimepungua zaidi na ukabila unaendelea kufifia pia. Wananchi sasa wanashikana mikono na kufanya harambee pamoja bila kujali dini, rangi, kabila wala sehemu watokayo. Miradi iliyo changiwa imezidi na pesa zilizo changwa pia zimekuwa ni za kuridhisha.

Siasa za Matuga sasa shuwari, watu wako huru na mawazo yao yanasikika na pia kuheshimiwa. Chuki imepungua, uhuru wa mawazo, wa kuabudu na kujumuika na wengine umehifadhiwa na kuendelezwa vilivyo.

Kina mama, vijana na wazee wana shirikiana kwa pamoja katika kuendeleza miradi yao na kujenga taifa la Kenya kuanzia mashinani. Na hii inadhihirishwa na ongezeko kubwa la michango ya miradi iliyofanyika mwaka huu.

### 1.2 MAENDELEO YA KIELIMU NA KIJAMII

Wale wanaojua wamejionea wenyewe jinsi elimu yetu ilivyostawi mwaka wa 2001. Watoto walio ingia shule za upili waliongezeka, wale walio enda vyuo vya kujifunza ualimu (Teacher Training Colleges) hao pia sasa ni wengi na wale walio kwenda vyuo vikuu – Nairobi University, Moi, Kenyatta, Jomo Kenyatta, Egerton na kadhalika - pia wameongezeka. Na hao wote mbunge ameweza kuwasaidia kulipa kiasi fulani cha karo kama inavyo onekana kwenye orodha zetu za karo hapo sehemu ya pili na tatu kwenye taarifa hii.

Baada ya miaka miwili hivi tutakuwa na ongezeko la walimu wetu wenyewe kutoka hapa Matuga waweze kusomesha shule za upili na za msingi pia. Mbunge amefanya juhudi hizi, ili kupunguza idadi ya walimu wa shule zetu kutoka sehemu nyengine za jamhuri yetu ya Kenya ndiposa utamaduni wetu upate kudumu.

Hata pia shule zetu zimefaidika na michango mbali mbali kama vile orodha zetu za sehemu ya pili na ya tatu zinavyo onyesha. Shule za upili za Ng'ombeni, Mkongani, Golini, Tsimba, Shimba Hills, Kichaka Simba, Mwaluphamba na Lukore zote zimepata usaidizi mwaka wa 2001. Hii ni dalili ya kuonyesha maendeleo ya kielimu kwenye eneo letu hili la Matuga.

Shule za msingi pia hazikusahaulika, kama vile orodha zetu kwenye sehemu ya pili na tatu ya taarifa hii hii zinavyokariri. Hata pia shule hizo ziliweza kupatiwa usaidizi wa fedha za vitabu baada ya mbunge kutia mkazo msaada huo uje kuwafadhili kutoka kwa serikali yetu tukufu. Kata ya Matuga ilipata kiasi cha shilingi Kshs. 940,000/= na ile kata ya Kubo ikapata shilingi Kshs. 750,000/= kununua vitabu vya shule kwenye sehemu zao. Haya sio mazuri?

Tumeweza pia kuanza kujenga chuo chetu cha wakunga – " Kwale Medical Training Centre" na tunatazamia kukikamilisha mwaka wa 2002, ili mwaka wa 2003 tuweze kusomesha watoto wetu kwenye chuo hicho. Watoto wetu watakapo hitimu kutoka chuo kama hicho, tutakuwa na wakunga (Nurses) na wasaidizi wa hospitali (Medical Assistants) wengi wa kutuhudumia.

Haya ni kati ya mambo ambayo mbunge wetu ametufikiria na kutuandalia. Huo ndio uongozi wa mbunge wetu wa sasa. Yote haya yapo na ni ya kweli, tupate uongozi gani zaidi ya hivi? Tushikane pamoja jamani!

Viwango vya usaidizi wa karo (Bursaries) vimezidishwa tukifananisha na tarakimu za miaka ya nyuma (angalia orodha sehemu ya pili na ya tatu) na ukarabati wa shule zenyewe umeendelea kote Matuga. Mitihani ya shule za msingi na za upili imepitwa vyema na watoto wengi wamefuzu kuendelea mbele. Hii ni kwa sababu shule sasa ni nzuri, madawati yapo, walimu wana motisha nzuri na wazazi nao wamezidi kuelewa na faida ya elimu ya watoto wao. Haya yote ni kwa ukombozi adilifu mbunge wetu aliotuahidi wakati alipo omba kura pale mwaka 1997. Jee una mengine ya kumshauri ili aongoze vyema? Yeye yuko tayari kukusikiliza.

Kwenye viwango vya usaidizi kwa vijana na kina mama mbunge amezidisha juhudi zake maradufu: misaada ya vikundi vya kina mama, vijana, misikiti na makanisa yaliyoko sehemu yake ya ubunge yamefaidika sana mwaka huu. Misaada hiyo pia inaweza kutambulika kwa urahisi kwenye ile orodha yetu iliyoko sehemu ya pili na tatu. Vilabu vya vijana wa mpira, vyama vya vijana vya kiuchumi pia vimeangaliwa na kustawishwa vilivyo.

Jee, haya si yale yale mliyo ahidiwa na mheshimiwa wakati alipo waomba kura mwaka 1997? Michezo ya "Kamolleh Cup" upande wa mpira wa mikono (Basketball) pia yameendelea kama kawaida. Kwa ufupi, maendeleo ya elimu yetu na ile ya watoto wetu imeimarika zaidi, miradi yetu ya akina mama, vijana na usaidizi wa karo umeenda mbele, na shuleni mwetu pia madawati yameongezwa.

Maendeleo yetu ya kielimu na kijamii yameenuka na yamepanda. Huo ndio mwelekeo wetu katika siasa yetu hii ya sasa. Hakuna wizi wa mashamba na pesa za jamii ni salama na watu wako huru na kufanya kazi pamoja wakiongozwa na mbunge wao mwenye kusikiliza matakwa yao , ushauri wao na kadhalika. Ni nini zaidi ya kupata mbunge kama huyu?

## 1.3 UPANUZI NA UTANDAZAJI WA MAJI KOTE

Ukombozi wa Matuga umeona na kuleta mwanzo wa upanuzi na utandazaji wa maji masafi kwa watu wa sehemu kame za eneo la ubunge. Vibanda (Kiosk) vya maji vimeenezwa hapa na pale kupitia wafadhili, na sehemu nyingine visima vipya vimechimbwa. Sehemu za Mwaluphamba, Mangawani na Mkongani zimefaidika. Tutaendelea na juhudi hizo mpaka kila mtu wa eneo la ubunge la Matuga awe ataweza kupata maji safi ya kutosha na karibu naye. Na vilevile mabwawa (Dams) mapya yatachimbwa huko Mkongani, Mbuguni Mangawani na Golini hivi karibuni ili maji zaidi yaweze kupatikana. Na sehemu zile za mienuko kama Lukore, Shimba Hills na Majimboni zitapata maji kupitia matangi ya kuhifadhia maji hivi karibuni. Kwa uwezo wake Mungu, na mipango ya serikali yetu, mambo haya yatatimizwa kwenye miaka miwili hivi. Juhudi hizi zote ametuandalia mbunge wetu. Ni furaha iliyoje kupata uongozi wenye upeo maridhawa kama huu? Heko kwa mbunge wetu na tuombe Mungu ampe afya njema ili azidi kutufikiria na kutufanyia mema zaidi ya haya.

## 1.4 UKARABATI WA BARABARA NA MADARAJA

Ukombozi wa Matuga ulikuja, navyo vitendo vikaonekana, wala sio maneno matupu. Ingawaje hali ya uchumi ni ngumu hata kwa serikali yetu tukufu,lakini ujasiri, hekima na ushauri bora wa mbunge wetu umeweza pia nasi kutuletea manufaa kwenye miundo – msingi yetu.
Hivi kwamba barabara zetu nyingi (Sio zote!) zimeweza kufanyiwa ukarabati madhubuti. Hii leo barabara zile za Kwale, Mangawani, Muhaka, Kona Masai, Shimba Hills, Mkelekeleni, Lukore katika kata ya Kubo zote zimeweza kutengenezwa ili wananchi waweze kusafiri vyema. Hata zile barabara za kata ya Matuga kama zile za Kwale Golini, Matuga – Tiwi, Check Point – Bombo mpaka Mbuguni na kadhalika zote hizi zimefanyiwa ukarabati wa kisawa sawa.

Wananchi wanaoishi huko wana furaha, wamefarijika kuweza kupata usafiri bila taabu. Mizigo na shehena zao zinaweza kufika pale watakapo bila tashwishi ya barabara mbaya. Hayo yote yamefanywa kuwa rahisi na ya kuridhisha, maana barabara nyingi ni poa. Ndugu zangu, siwezi kujisifu kwa hayo bali ninayo furaha tele kuweza kuwahudumia namna hii.

Daraja zile zote ambazo zilikuwa zimeharibiwa na mvua kuu ya "EL NINO", zimeweza kutengezwa upya na kufanyiwa ukarabati wa kutosha. Haya yasiwe yanaonekana kuwa yalikuja kibahati bali ni juhudi za mbunge wetu, mkombozi. Maendeleo ya sehemu yoyote ile hayakamiliki mpaka miundo msingi (Infrastructure) ya sehemu hiyo iwe ya kuridhisha. Miundo msingi muhimu kwetu sisi ni kama vile barabara, maji, simu, taasisi za elimu, taasisi za afya na mwisho kabisa ni umeme wa spaki. Tumetia mkazo zaidi kwa barabara zetu, simu zinapatikana kote Matuga, lakini hata hivyo tutaongeza. Tumeweza pia kutekeleza utandazaji wa maji sehemu nyingi, na hapa pia hatuja kamilisha mradi huu. Kwenye taasisi za elimu tumepiga hatua ndefu na maridhawa, na taasisi za afya bado hazijatimia tutakavyo, hasa sehemu zile za mienuko ya Shimba Hills, Mwaluphamba na Mkongani.

Mwaka ujao wa 2002 tutatilia mkazo zaidi yale mambo ya maji, taasisi za afya na hasa kwa umuhimu wa hali ya juu umeme wa spaki, (Electricity). Tuombe mungu tuwe na afya njema na tuzidishe juhudi zetu kuona kua miradi hii inaanzishwa hata kama haitamalizika mwaka huo wa 2002.
Ndugu zangu wa Matuga, haya si mengi yaliyo tendeka, na wala si machache pia kulingana na hali ilivyo ya kiuchumi humu nchini Kenya. Jee, haya yatawaridhisha kwa sasa au kuna mengine ya kuongeza ? Semeni msikike !!

## 1.5 MAENDELEO YA KIUCHUMI.

Kwenye taarifa yetu ya mwaka wa 2000, ukurasa wa sita (6), tulisema ya kwamba "...***kwenye mkondo wa harakati za maendeleo ya kiuchumi, hatutasita mpaka tuone kua maisha ya watu wetu yanabadilika kuwa bora kila mwaka"***. Na tulisema pia yakwamba ***"...mawasiliano mema na uchukuzi mzuri wa abiria na mizigo yetu itaimarishwa ..."***. Tumeona kwenye taarifa hii ya mwaka 2001 vile shule zetu, barabara zetu, utandazaji wa maji na mengineyo yalivyoweza kuboreshwa ili kuhimili maisha bora ya wananchi. Hivi ndivyo ukweli wa mambo ulivyo !
Utalii umeanza kufunguka, nayo makazi pia yameanza kupatikana, ijapokuwa hayatoshelezi kwa kila mtu. Ni haba na haba mpaka kujaza kibaba. Wachuuzi wa nyama, matunda, mboga, nafaka na mengineyo wameanza kufanikiwa ijapo kidogo.

Sio kama vile mwaka wa 2000 ulivyokua. Mambo bado ! Tumepigania wajengaji (Kandarasi) wadogo wa barabara nao wapewe nafasi, angaa wajipatie riziki, na kuwanufaisha watu wa kazi za mkono. Haya yote ni kusaidia uchumi uende pia kwa mifuko midogo ya wananchi wa vijijini. Hatujafanikiwa kikamilifu na hatujapata matarajio yetu yote, lakini tofauti ipo nasi tumshukuru Mungu kwa kile kidogo tulichoweza kukipata wakati huu.

Sisi hatutachoka, wala hatutatosheka kwa haya, bali tutaongeza juhudi vilivyo na tutashughulika kwa kujitolea muhanga mpaka tuone ufanisi kamili umepatikana.

Kule Shimba Hills uchimbaji madini ya "Titanium" tumeweza kusimamisha,hadi masharti yetu yakubaliwe. Tutakubali uchimbaji huo iwapo tu pingamizi za yale masharti yetu yakubalika, haya ni:-

- Wakazi wa sehemu zenye madini, na Kwale kwa jumla wapewe hisa (shares) zenye asili mia ishirini (20%) ya thamani ya kampuni itakayo chimba madini hayo.

- Ukuzaji wa uchumi wetu uambatane na uchimbaji wa madini hayo ya "Titanium", hivi kwamba madini hayo yachimbwe, yasafishwe na yauzwe kutoka hapo yalipo. Hatutakubali usafirishaji mchanga (Ore)wala madini hayo kwenda kwengineko kabla hayaja lipiwa thamani yake pale yalipo, hapa kwetu Kwale.

- Kampuni ya "Tiomin" au yoyote ile wakubali taarifa ya utafiti nyengine na mpya itolewe na ambayo itaonyesha maafa, na madhara yanayoweza kupatikana kwa watu wetu wakati wa uchimbaji madini hayo. Madini haya yanatoa cheche za miale ambayo inaweza kutudhuru sana miili yetu.

Serikali nayo imekubali kutafakari zaidi juu ya masharti au maazimio hayo yetu. Tulipata ushindi kwenye mahakama, na sasa imebaki uamuzi wa muongozo wa serikali yetu. Iwapo tutafaulu, basi tutaweza pia kupata tija maridhawa, maana madini hayo yana thamani ya kiasi cha shillingi billion 855 na endapo tutapata asilimia ishirini (20%) basi hizo ni fedha nzuri za kutuwezesha kujimudu kwa siku nyingi wilayani Kwale. Tuombe Mungu maombi yetu yasikizwe na yakubalike !

Upande wa mazao yetu ya kilimo haujapata nafuu bado. Nazi zetu na vifaa vinavyotolewa kutokana na mti wa mnazi haujalete manufaa tunayotarajia. Majadiliano zaidi yafaa kufanyika ili tupate mwelekeo ufaao. Haya ni mambo ya sisi sote kwa pamoja – wasomi, walimu, wazee, vijana, kina mama – sote kama tulivyo !

Mazao ya machungwa yameimarika vizuri lakini soko la kuuza Machungwa hayo bado limekosekana. Kwa muda mrefu sasa tumetegemea kupeleka mazao yetu **KONGOWEA**. Soko hilo limejaa mazao ya Naivasha, Tanga na mengineyo. Machungwa yetu bado yananunuliwa kwa bei duni, nasi tunaumia kwenye ubwanyenye huo kwenye soko hilo. Suluhisho ni kupata njia ya soko jipya. Soko kama

hilo tayari limeanza kujengwa huko Ukunda ili kufaidi wale wakulima walioko sehemu zetu. Itatubidi pia tuweze kutengeneza asiri (Juice) ya machungwa, hata bila ya mtambo ili tuweze kuuza asiri hizo kwenye mahoteli na mikahawa mbali mbali katika sehemu zetu za pwani.

Mazao ya Bixa yameumiza wakulima wetu kwa muda mrefu sana. Wakulima wametia bidii, wamejizatiti vilivyo lakini mnunuzi ni mmoja (Kenya Bixa) naye bei zake ni za kulaghai na kuwapunja wakulima wetu. Suluhisho lipo tu kwa njia ya mabadiliko ya sheria ili wanunuzi wengi waweze kukubaliwa nao waweze kushindana katika kununua bidhaa hizo ndiposa bei ya zao hilo iweze kuimarika vilivyo, nao wakulima wetu waweze kuponea na kufaidika.

Zao la korosho kwenye mkondo wa mwambao wa ubunge halijawa la kuleta tija pia. Ingawaje kiwanda cha korosho kilichoko Kilifi kimefungwa na hivyo hakiwezi kutumia na kuenua zao hili, kuna wachuuzi wengi wa kibinafsi ambao hununua zao hilo. Pingamizi katika zao la korosho liko katika uzalishaji wenyewe. Mikorosho imekuwa mizee, na pia ugonjwa wa wadudu fulani umekumba miti yetu ya mikorosho.

Kuna utafiti unaoendelea na kuna mbinu za kuweza kunyunyuzia dawa mikorosho, ndiposa wadudu hao waweze kuangamizwa, ili mikorosho iweze kuzaa tena. Hivyo basi, wakati serikali inatuhudumia kwa njia ya ule utafiti unao endelea, na unyunyuzaji wa dawa utakao anza, ni jukumu letu sisi wakulima nasi kuweza kuiondoa ile miti mizee ya mikorosho, na tupande miche mipya kwa mazao bora mbeleni. Ndugu zangu, tujitayarishe leo ili tufaidike kesho.

Viongozi wameandaa kupeleka miswada Bunge ili haya mazao yetu yote – Nazi, Korosho na Bixa – yaweze kupata halmashauri zao. Yaani tuweze kuwa na halmashauri ya mazao ya mnazi –" Coconut Board of Kenya" na vilevile "Cashewnut Board of Kenya". Iwapo halmashauri hizo zitaweza kubuniwa zitasaidia sana kukuza mazao hayo yetu. Upande wa upandaji, uvunaji na uuzaji wa mazao haya yataweza kushughulikiwa na halmashauri hizo. Hata hivyo haya ni mambo ya baadaye na sisi lazima tujizatiti vilivyo tuweze kufanya tuwezavyo kwa sasa mpaka wakati huo utakapofika.

## 1.6 USITAWI WA USALAMA NA AMANI

Katika taarifa zetu za miaka mitatu iliyopita, tulizungumzia juu ya ghasia na fujo zilizokuwepo katika mwaka wa 1997, ambapo vita vya ujambazi vilizuka. Vita hivi viliharibu mambo mengi ya kiuchumi na kijamii, kama tulivyo kariri hapo mbeleni. Jitihada za kutuliza vita hivyo zilifuzu nasi tuko katika hali ya usalama na amani.

Kuanzia mwaka wa 1999, eneo letu lilirudi katika hali yake ile ya zamani. Leo maafa yaliyotukumba yamefifia, watu sasa wanaishi kwa amani. Hakuna tena watu wa kuhama hama, wala wanajisiwa, wala kuuwawa. Wakulima wanaendelea na makazi yao na wachuuzi vile vile. Walimu na wanafunzi wamekaa poa, masomo moto moto, elimu yaendelea na ufanisi kupatikana. Yote hayo yaliyo tupotezea thamani ya zaidi ya milioni hamsini (50 million) yamekwenda.

Kulingana na usalama tulio nao sasa, utalii nao umeanza kuenuka, makazi yanapatikana, wakulima wanauza mazao yao na huduma za malazi (Accomodation) pia yameanza kutumika na kuleta fedha kwa wale wenye nyumba na hoteli zao kwenye eneo letu.

Serikali nayo imeongeza huduma za usalama katika eneo letu na wale walinzi wa vijijini (Tsungutsungu) katika tarafa zetu wamefanya kazi nzuri pia. Zile sehemu ambazo zilikuwa na fujo na ghasia pia sasa zimeweza kutulia. Ninawapongeza sana wafanyikazi wa utawala wilayani – Ma- D.C., D.O, Chifu na Chifu wadogo kwa kuhimili usalama huo ambao imewezesha wananchi kufanya kazi zao kwa amani na utulivu. Haya nayo pia ni maendeleo makubwa kwetu sisi maana maisha yetu yanalindwa nao usalama unatuwezesha kufanya kazi zetu.

Kwa mara nyingine tena, ningependa kuwaomba watu wote wa Matuga walinde na kudumisha amani hii tuliyo nayo kwa dhati, ili tuweze kuendelea, isije amani hii ikatuponyoka tena na tukarudi katika hali ya ghasia, fujo na mihangaiko ile ya zama za 1997. Ndugu zangu, tuliyoyapoteza ni mengi na siasa za ghasia na ujambazi, ni siasa duni, za kishenzi na kinyama. Hatutaki kupoteza tena watoto wetu, ndugu zetu, vipenzi vyetu katika ghasia kama ile iliyotukumba zama zile. Kosa lile tulilolifanya siku zile tusilirudie tena katu !

Kwa haya tuliyosema juu ya usalama, ningependa pia kuwahimizeni watu wa Matuga, tuache kuoneana wivu, ambacho mara nyingi ndio chanzo cha rabsha. Tuache kuzurura kiholela, hasa vijana, maana hata mambo kama haya hufanya watu kushawishika kuanza ghasia bila sababu yoyote.

Siwezi kukataza watu mambo fulani fulani, lakini moja ya maafa makubwa yanayoweza kuleta ukosefu wa usalama ni utumiaji wa madawa ya kulevya (Drugs)! Vijana wetu wametiwa kwenye janga hili bila wao kujua madhara, na leo wengi wao wanatumia madawa haya. Tujiepushe nayo, na wazazi, walimu na watu wenye majukumu katika jamii zetu, wote pamoja wajaribu kuwasaidia vijana wetu, wake kwa waume. Tuungane pamoja tujiepushe kwa haya nasi tutafaulu kwenye mambo yetu mengi.

# SEHEMU YA PILI (II)

## 2.0 HARAKATI ZA MBUNGE KUENEZA NA KUKUZA MAENDELEO NA PIA MIRADI ILIYOCHANGIWA KWA MUHTASARI MWAKA WA 2001

| TAREHE | SEHEMU | MIRADI YENYEWE ILIYO CHANGIWA | RUZUKU ZA MBUNGE | MICHANGO JUMLA YAKE |
|---|---|---|---|---|
| 3/1/2001 | Mangawani | Msaada wa vitabu kwa shule saba (7) | 56,000/= | 213,000/= |
| 6/1/2001 | Ofisi | Misaada mbali mbali | 8,000/= | 8,000/= |
| 7/1/2001 | Tiwi | Msaada kwa akina mama | 9,000/= | 9,000/= |
| 8/1/2001 | Shimoni | Mchango kwa kura ya udiwani (KANU) | 5,000/= | 5,000/= |
| 9/1/2001 | Majoreni | Mchango kwa kura ya udiwani (KANU) | 10,000/= | 10,000/= |
| 10/1/2001 | Msambweni | Mchango kwa kura ya udiwani (KANU) | 15,000/= | 15,000/= |
| 11/1/2001 | Kidimu | Mchango kwa kura ya udiwani (KANU) | 10,000/= | 10,000/= |
| 20/1/2001 | Golini | Misaada kwa wananchi | 5,000/= | 5,000/= |
| 21/1/2001 | Mwaluphamba | "KAMOLLEH CUP" PARTY-Hafla ya ushindi | 25,000/= | 169,000/= |
| 22/1/2001 | Tsimba | Ruzuku kwa shule yao ya upili. | 100,000/= | 100,000/= |
| 28/1/2001 | Matuga | Mchango wa msikiti | 15,000/= | 39,000/= |
| 4/2/2001 | Tiwi | Kikundi cha vijana wa mpira-mshale | 35,000/= | 48,000/= |
| 4/2/2001 | Tiwi | Mchango kwa vikundi vya akina mama wote | 100,000/= | 710,000/= |
| 25/1/2001 | Matuga (Waa) | Mchango kusaidia mchezo wa mpira | 10,000/= | 10,000/= |
| 26/2/2001 | Matuga (DDI) | Kamati ya kupambana na ugonjwa wa ukimwi | 3,000/= | 3,000/= |
| 11/3/2001 | Ofisi | Msaada mbali mbali | 15,000/= | 15,000/= |
| 17/3/2001 | Boyani (Majimboni) | Vikundi vya akina mama (Mchango) | 35,000/= | 220,000/= |
| 18/3/2001 | Matuga Girls (Waa) | Mchango kusaidia shule ya wasichana | 20,000/= | 80,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19/3/2001 | Matuga (DDI) | Kamati ya kupambana na ugonjwa wa ukimwi | 5,000/= | 5,000/= |
| 24/3/2001 | Kwale | Maadhimisho ya kamati ya kupambana na ugonjwa wa ukimwi | 79,000/= | 79,000/= |
| 31/3/2001 | Kichaka Simba (Mwaluphanga) | Mchango kusaidia shule ya wasichana | 63,000/= | 63,000/= |
| 1/4/2001 | Ofisi | Misaada mbali mbali kwa wananchi | 15,000/= | 15,000/= |
| 2/4/2001 | Lukore | Msaada kwa waimbaji wa shule ya Lukore | 4,000/= | 4,000/= |
| 7/4/2001 | Tiwi | Hafla ya Kiweke FC juu ya "Kamolleh Cup" | 30,500/= | 35,000/= |
| 8/4/2001 | Tsimba | Mchango kusaidia vikundi vya kina mama | 49,000/= | 98,000/= |
| 9/4/2001 | Lukore (Mkanda III) | Msaada kwa miradi ya Mkanda III | 10,000/= | 10,000/= |
| 22/4/2001 | Matuga (MTC) | Msaada kwa shule ya ukunga (MTC) | 10,000/= | 10,000/= |
| 28/4/2001 | Vuga (Tsimba) | Msaada wa msikiti wa Chirimani (Vuga) | 15,000/= | 15,000/= |
| 12/5/2001 | Ofisi | Msaada kwa watu mbali mbali ofisini | 20,000/= | 20,000/= |
| 13/5/2001 | Burani (Mwaluphamba) | Mchango wa shule ya upili ya huko | 60,000/= | 400,000/= |
| 13/5/2001 | Burani (Mwaluphamba) | Msaada wa Burani Primary School | 50,000/= | 50,000/= |
| 19/5/2001 | Taita | Mchango kusaidia vikundi vya akina mama Mwatate | 50,000/= | 590,000/= |
| 26/5/2001 | Mangawani | Mchango wa bursary kusaidia karo za shule | 75,000/= | 360,000/= |
| 2/6/2001 | Tiwi | Mashine za kushonea nguo kwa akina mama thamani ya zote tatu | 33,000/= | 33,000/= |
| 3/6/2001 | Ofisi | Msaada mbali mbali kwa wananchi | 9,500/= | 9,500/= |
| 7/7/2001 | Zimbabwe F.C (Waa) | Hafla yao ya ushindi wa kikombe (Misaada) | 30,000/= | 60,000/= |
| 8/7/2001 | Ng'ombeni | Misaada kwa shule mbali mbali - ZAWADI | 30,000/= | 30,000/= |
| 15/7/2001 | Waa | Mchango kusaidia vijana (Youth) wa Waa | 43,000/= | 155,000/= |
| 22/7/2001 | Majimboni | Mchango kusaidia akina mama wa vikundi | 100,000/= | 450,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 28/7/2001 | Ng'ombeni | Mchango kusaidia shule ya upili ya Ngo'mbeni | 60,000/= | 890,000/= |
| 4/8/2001 | Mwingi | Mchango kusaidia shule ya upili ya wasichana Mwingi | 25,000/= | 680,000/= |
| 18/8/2001 | Waa | Mchango kusaidia vikundi vya kina mama | 108,000/= | 573,000/= |
| 19/8/2001 | Kizibe (Mwaluphamba) | Mchango kusaidia shule ya msingi | 30,000/= | 110,000/= |
| 26/8/2001 | Tiwi | Mchango wa msikiti huko Tiwi Chai | 30,000/= | 150,000/= |
| 8/9/2001 | Mwaluphanga Catholic Church | Msaada kujenga kanisa upya | 10,000/= | 29,000/= |
| 9/9/2001 | Ofisi | Msaada kwa wananchi | 25,000/= | 25,000/= |
| 16/9/2001 | Ng'ombeni | Mchango kusaidia kina mama na vikundi | 15,000/= | 50,000/= |
| 22/9/2001 | Kwale | Viburudisho kwenye mkutano wa Kanu | 5,000/= | 5,000/= |
| 23/9/20011 | Golini | Mchango wa zahanati ya Chitsanze | 78,000/= | 115,000/= |
| 25/9/2001 | Tiwi | Msaada wa ununuzi wa miche ya miti | 10,000/= | 10,000/= |
| 29/9/2001 | Likoni | Mchango wa Likoni | 10,000/= | 10,000/= |
| 29/9/2001 | Tiwi | Msaada wa Ijtmai | 10,000/= | 10,000/= |
| 30/9/2001 | Kwale | Mchango wa vikundi | 80,000/= | 286,000/= |
| 1/10/2001 | Kichaka Simba (Mwaluphanga) | Msaada kwa wananchi huko | 15,000/= | 15,000/= |
| 6/10/2001 | Ofisi | Misaada kwa wananchi | 10,000/= | 10,000/= |
| 7/10/2001 | Lukore | Misaada ya karo | 40,000/ | 40,000/= |
| 21/10/2001 | ZIBANI (Ng'ombeni) | Mchango wa msikiti | 50,000/= | 180,000/= |
| 27/10/2001 | Waa | Msaada wa karo | 95,000/= | 510,000/= |
| 3/11/2001 | Majimboni | Mchango wa vikundi | 100,000/= | 360,000/= |
| 4/11/2001 | Vuga (Tsimba) | Msaada wa shule | 24,000/= | 45,000/= |
| 9/11/2001 | Nyatike (Kisii) | Msaada wa zahanati | 10,000/= | 210,000/= |
| 10/11/2001 | Malindi | Mchango wa shule | 25,000/= | 25,000/= |
| 11/11/2001 | Voi (Taita) | Mchango wa Karo | 8,000/= | 460,000/= |
| 12/11/2001 | Kichaka Simba (Mwaluphanga) | Mchango wa shule ya wasichana | 15,000/= | 120,000/= |
| 18/11/2001 | Mwanamkuu (Mwaluphanga) | Mchango wa kanisa | 19,000/= | 90,000/= |
| 24/11/2001 | Ofisi | Misaada kwa wananchi | 20,000/= | 20,000/= |
| 25/11/2001 | Mwaluphamba | Mchango kwa shule saba | 108,000/= | 786,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1/12/2001 | Samburu (Kinango) | Mchango wa makanisa | 25,000/= | 180,000/= |
| 2/12/2001 | Miyani (MTC) Golini | Mchango wa shule ya ukunga | 15,000/= | 155,000/= |
| 30/12/2001 | Ofisi | Misaada kwa wananchi | 10,000/= | 10,000/= |
| 3/1/2002 | Ofisi | Msaada wa usafiri kwa wanachama wa KANU | 4,000/= | 4,000/= |
| 5/1/2002 | Msambweni | Mchango wa vikundi vya kina mama | 45,000/= | 139,000/= |
| | | | | |
| | **Jumla Ndogo** | **Michango iliyochangiwa** | **2,400,000/=** | |
| | **Jumla zote** | **Michango yote ya mwaka** | | **10,740,512/=** |

# SEHEMU YA PILI (II)

## 2.1 TAHLILI YA NYENDO ZA MBUNGE AKITANDAZA MIFUMO YA MAENDELEO KATIKA SEHEMU YAKE YA UBUNGE YA MATUGA

| TAREHE | SEHEMU | YALIYOTENDEKA MWAKA WA 2001 |
|---|---|---|
| 3/1/2001 | Mangawani | Kwa mwaliko wa wazazi na diwani wa sehemu hiyo, mbunge alikwenda Mangawani kuchangia mfuko wa shule saba (7) za msingi ili waweze kununua vitabu vya shule, kusaidia gharama kwa wazazi hao. Hapo mbunge alitoa mchango wake wa Kshs. 56,000/=, na jumla ya mfuko huo ukafika kiasi cha Kshs. 213,000/= |
| 6/1/2001 | Ofisi (Denyenye) | Mbunge aliendelea kuona watu wanaokuja kumtembelea kwa mintarafu mbali mbali, naye akaweza pia kusaidia watu aina mbali mbali. Hapo aliwasaidia pia vijana wa Denyenye wenye mradi wao Kshs. 3,000/=. Akina mama wa Itambia Group Kshs. 2,000/=, Kichaka Simba Women Group Kshs. 2,000/=, Katangini Youth Group Kshs. 1,000/= na kadhalika. |
| 7/1/2001 | Tiwi (Mwaligulu School) | Mbunge aliitwa na akina mama wa Tiwi Women Groups kukutana nao kwa minajili ya kupanga harambee yao ya vikundi vyote vya Tiwi. Baada ya mazungumzo hayo, mbunge aliwaruzuku kina mama kwa Kshs. 9,000/= za mkao. |
| 8/1/2001 | Shimoni (Msambweni) | Baada ya kifo cha diwani wa KANU huko Pongwe-Kidimu, mbunge alilazimika kwenda eneo la ubunge la Msambweni, kusaidia chama, katika matayarisho ya kura ndogo (By-election). Mbunge aliruzuku kiasi cha Kshs. 5,000/= kusaidia mambo mbali mbali katika shughuli hizo, wakiwa pamoja na waheshimiwa Marere na Mkalla. |
| 9/1/2001 | Majoreni (Msambweni) | Baada mkutano wa siasa wa Shimoni, Mbunge alihudhuria mkutano mwengine wa matayarisho ya kura hiyo ya sehemu ya Pongwe-Kidimu huko Majoreni. Kwenye mkutano huo mbunge aliruzuku kiasi cha Kshs. 10,000/= kusaidia mambo mbali mbali wakiwa pamoja na wabunge wote wa Kwale. |
| 10/1/2001 | Tswaka (Msambweni) | Kwenye matayarisho hayo ya kura za huko, mkutano mwingine ulifanyika Tswaka, ambako wabunge hao walijizatiti kusaidia chama chao cha KANU kushinda uchaguzi huo. Mbunge aliruzuku kiasi cha Kshs. 15,000/= kusaidia mambo mbali mbali ya harakati hizo. |
| 11/1/2001 | Kidimu (Msambweni) | Mkutano huo wa mwisho kutayarisha uchaguzi huo ulifanyika Kidimu. Wabunge waliungana tena na wakafanya kazi vilivyo. Hapa mbunge aligharamia mambo haya kwa kiasi cha Kshs. 10,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 14/1/2001 | Arusha (Tanzania) | Kama mwana kamati ya Bunge inaayohusika na uhusiano wa Kenya na nchi za nje, mbunge alialikwa kwenda kuadhimishwa kwa ule umoja wa Afrika Mashariki (East African Community) ambako maraisi (Moi, Mkapa na Museveni) wa nchi hizo tatu waliweka sahihi ya maadhimisho hayo. |
| 20/1/2001 | Golini | Mbunge alikwenda Golini pamoja na mwenziwe mheshimiwa Mkalla wa Kinango, kuhudhuria mkutano wa wakulima na wakurugenzi wa Hifadhi ya Ndovu ya Mwaluganje (Mwaluganje Elephant Sanctuary). Wakulima walilalamika sana kwamba mimea yao inaharibiwa na ndovu nao wakurugenzi hawakuonekana kama wanajali uharibifu huo. Baada ya majadiliano marefu suluhisho lilipatikana na wakaafikiana juu ya ua wa kuzuia ndovu hao wasingiie mashambani mwa wakulima. Mkutano huo pia ulihudhuriwa na D.O. wa Matuga. |
| 21/1/2001 | Mwaluphamba | Mbunge alisafiri kwenda tarafa ya Mwaluphamba kuhudhuria hafla ya vijana wa mpira kusherehekea ushindi wao wa kombe la "Kamolleh Cup". Kwenye mchango wao hapo, mbunge aliwaruzuku kiasi cha Kshss. 25,000/= nao wakapata jumla ya Kshs. 169,000/=. |
| 22/1/2001 | Tsimba | Kwa hali ya shule yao ya upili ilivyokua na matatizo ya ujenzi ili kumaliza sehemu za muhimu, mbunge alikwenda huko na akawapa ruzuku ya kiasi cha Kshs. 100,000/= ili waweze kumaliza majengo hayo yao. Kamati na wananchi walishukuru nao waliweza kusaidika vilivyo. |
| 25/1/2001 | Nairobi | Mbunge alisafiri kwenda Nairobi kuhudhuria kikao chaa kamati ya Bunge ya "Ulinzi na Uhusiano wa Kimataifa" |
| 28/1/2001 | Matuga | Mbunge alialikwa harambee ya msikiti wa Matuga karibu na ofisi ya D.O. Mbunge alitoa ruzuku ya kiasi cha Kshs. 15,000/= kupitia D.O. wa Matuga. |
| 1/2/2001 – 2/2/2001 | Kwale | Kwa sababu ya kutoeleana ambako kulileta vurugu kati ya wakulima wa Shimba Hills na kampuni ya "Tiomin Inc." Ya Canada kuhusu uchimbaji wa madini ya "Titanium" huko Nguluku na Mivumoni, mbunge aliialika Kamati ya Bunge inayohusika na Kilimo, Madini na Mali ya Asili, ili kuja kutatua vurugu hilo. Serikali ilifunga uchimbaji huo mpaka masikizano kamili. |
| 3/2/2001 | Shimba Hills | Mbunge alisafiri kwenda tarafa ya Majimboni katika ofisi ya D.O. ya Shimba Hills ambako alihutubia baraza. Huko mambo ya uchimbaji madini ya Titanium yalijadiliwa, mambo ya barabara na elimu kwa jumla yalipewa msitari wa mbele. Mbunge alitatua hayo jinsi walivyotarajia. |
| 4/2/2001 | Tiwi | Mbunge aliendа tarafa ya Tiwi kuhudhuria hafla ya vijana wa mpira waliokua wanasherehekea ushindi wao wa kikombe cha mpira. Vijana hao wa "Mshale Football Club" walishinda wengine wengi kupata kombe hilo. Katika hafla hiyo, mbunge aliwatunukia ruzuku ya Kshs. 20,000/= na akawapelekea ngoma ya "New Star" kwa Kshs. 10,000/= na vile vile "Uniform" za |

| | | |
|---|---|---|
| | | kuchezea mpira zenye gharama ya Kshs. 15,000/= . Kwa jumla mbunge aliwasaidia na kiasi cha Kshs. 35,000/=. Hafla yenyewe iliweza kuchangisha Kshs. 48,000/= siku hiyo. |
| 5/2/2001 | Tsimba | Mbunge alisafiri kwenda tarafa ya Tsimba pamoja na madiwani Ndalana (Majimboni) na Bandari (Tsimba) huko Tangini kuhudhuria baraza pamoja na D.C. wa Kwale, OCPD, DCIO na wengineo. Mzozo wa mpaka kati ya tarafa ya Majimboni na Tsimba ulizungumzwa kwa kirefu. D.C. wa Kwale akatoa uamuzi kuhusu mpaka ulivyo kati yao. |
| 8/2/2001 | Nairobi | Mbunge alihudhuria mkutano wa ile Kamati ya Bunge inayohusika na Usalama na Uhusiano wa Kenya na nchi za nje. Mkutano ulijadili mambo mbali mbali ya usalama wa nchi, na uhusiano wetu huko ng'ambo. |
| 13/2/2001 | Nairobi | Mbunge alihudhuria mkutano mwengine tena wa kamati hiyo wakiwa na wageni kutoka Ethiopia, wakiwemo mkuu wa majeshi ya huko, waziri wao wa mambo ya nje na balozi wao hapa Kenya. Mkutano ulijadili mambo mengi ya usalama na mambo ya kibalozi ya nchi hizo mbili. |
| 17/2/2001 | Majimboni (Shimba Hills) | Mbunge alihudhuria baraza huko Shimba Hills, ambako mambo ya mipaka ya tarafa pia yalizungumziwa. Usalama wa wananchi pamoja na mbinu tofauti za kuleta maendeleo pia zilipangwa. |
| 18/2/2001 | Golini | Mbunge alitembelea sehemu ya Golini baada ya kukutana na watu mbali mbali hapo ofisi. Huko Golini mbunge alikagua sehemu ile ambayo ule ua wa ndovu unatarajiwa kuwekwa na wafadhili utakavyopitia. Hata hivyo kumekuwa na kutoeleana kati ya wakulima na wakurugenzi wa Hifadhi ya Ndovu ya Mwaluganje (Elephant Sanctuary) kuhusu ua huo wa kuzuia ndovu wasiingie kwenye mashamba. |
| 24/2/2001 | Tiwi | Mbunge aliwaalika waheshimiwa Zipporah Kittony, Simeon Mkalla, Seif Kajembe, Basil Mwakiringo, Kihika Kimani na D.C. wa Kwale katika mchango wa kuchangia kina mama wote wa Tiwi kwenye vikundi vyao mbali mbali. Mchango huo ulipata kiasi cha Kshs. 710,000/= ukiwepo mchango wa Kshs. 70,000/= wa Hon. Kittony, mwenyekiti wa Maendeleo ya Wanawake Kenya, Kshs. 100,000/= wa Hon. Kimani na Kshs. 100,000/= wa mbunge wetu wa Matuga. |
| 25/2/2001 | Matuga Girls School | Mbunge alihudhuria kwenye mapambano ya kombe la mpira wa vikapu (Basketball) liitwalo "Kamolleh Basketball Cup". Michuano ilikuwa mikali kati ya timu za vijana kutoka Kwale na Mombasa. Hapo mshindi alipewa ruzuku ya Kshs. 10,000/= na mbunge wetu. Kabla ya kwenda kwa mchuano huo, mbunge alikutana na watu mbali mbali ofisini kama kawaida yake. |
| 26/2/2001 | Matuga, DD1 | Mbunge alienda Matuga ofisi ya D.O. na hapo akakutana na ile kamati yake ya kupambana na ugonjwa wa Ukimwi. Kamati hiyo iliyoundwa kutoka sehemu zote za eneo la ubunge la Matuga, |

| | | |
|---|---|---|
| | | imepewa jukumu la kutafuta mbinu za kupambana na ugonjwa huo mbaya. Mbunge alitoa Kshs. 3,000/= kwa viburudisho kwa wanakamati hao. |
| 27/2/2001 | Nairobi | Mbunge baada ya kukutana na kamati hiyo alisafiri kwenda Nairobi ambako alikutana na mkurugenzi mkuu anayehusika na halmashauri ya kupambana na ugonjwa wa ukimwi Dr. Mohammed Abdalla kwake ofisini. Walijadiliana jinsi kamati hiyo ya Matuga itakavyo adhimishwa. Nao wakampatia mbunge wetu vifaa vya kufanya matangazo katika kupambana na ugonjwa huo. |
| 5/3/2001 | Mombasa | Kama mwandishi wa umoja wa wabunge wote wa pwani (CPG) mbunge aliitisha na pia kuhudhuria mkutano wa kundi hilo la wabunge. Huko walijadili kwa kirefu mambo ya Kilindini, barabara ya Dongo Kundu na mengineo. |
| 10/3/2001 | Matuga | Mbunge alikutana tena na kamati yake ya kupambana na ugonjwa wa ukimwi kupanga siku ya kuadhimisha na kutawazwa kwa kamati hiyo kirasmi. D.O. wa Kubo na Matuga wote walikuwapo na wanachama wa kamati hiyo. Mipango ilifanywa ya kukaribisha wageni kwenye maadhimisho hayo. Baada ya mkutano huo asubuhi, Mbunge alisafiri kwenda Boyani (Majimboni Location) kukutana na akina mama wa huko ili kupanga harambee ya vikundi. |
| 11/3/2001 | Ofisi | Mbunge kama kawaida yake alikutana na wananchi katika ofisi iliyo Denyenye. Watu wengi kutoka sehemu mbali mbali walikuja kumuona na kujadili mambo yao ya vikundi ya miradi, na hata pia yale ya kibinafsi. Mbunge siku hiyo aliweza kusaidia watu kwa kiasi cha Sh.15,000/=. |
| 12/3/2001 | Ng'ombeni | Mbunge akiandamana na D.C. wa Kwale walitembelea miradi ya tarafa ya Ng'ombeni, kama vile kichinjio cha Pungu (Slaughter House) na shamba la ng'ombe wa maziwa la Hussein Dairy. Baadaye kuwahutubia wananchi na kusikiza matarajio yao kwa serikali. |
| 17/3/2001 | Boyani (Maji mboni Location) | Mbunge akiandamana na Diwani wake wa Majimboni wa sehemu hiyo (Ndalana) walitembelea Boyani tena na kuhudhuria mchango wa vikundi vya akina mama. Mchango huo ulipata fedha kiasi cha Kshs. 220,000/= naye mbunge akatoa mchango wake wa Kshs. 35,000/= kusaidia mradi huo. |
| 18/3/2001 | Waa (Matuga Girls) | Mbunge alialikwa kwenye mchango wa kusaidia shule ya wasichana ya Matuga Girls. Katika mchango mdogo huo wa kusaidia maji ya shule hiyo, kiasi cha Kshs. 80,000/= zilichangwa. Naye mbunge akasaidia kwa Kshs. 20,000/=. |
| 24/3/2001 | Kwale | Akiwa na wageni wake kutoka Nairobi, Dr. Mohammed Abdalla, D.C. wa Kwale, viongozi mbali mbali, wananchi na kadhalika, mbunge alihudhuria hafla ya kuadhimisha kamati yake ile ya kupambana na ugonjwa wa Ukimwi. Ngoma, tafrija, hutuba murua na vyakula vilivyo andaliwa, yalikuwa baadhi ya yale |

| | | |
|---|---|---|
| | | yaliyotokea siku hiyo. Halaiki kubwa ilihudhuria na hata kutojali mvua iliyo kuwako. Kusaidia hafla hiyo mbunge alitumia kiasi cha Kshs. 79,000/= kwa usafiri, ngoma, viburudisho, vyakula na mengineyo. |
| 25/3/2001 | Ofisi | Mbunge alikutana na watu tena hapo ofisini ili kusikiza matatizo, maagizo, na miongozo kutoka kwa watu wake kutoka sehemu mbali mbali za eneo lake la ubunge. Hapo aliweza kusaidia wananchi mbali mbali kwa kiasi cha Kshs. 10,000/= |
| 26/3/2001 | Kwale | Mbunge alihudhuria kikao cha wilaya kinacho shughulika na mipango ya maendeleo (DDC). Mengi yaliyojadiliwa na mipango kuhusu maji, barabara, shule, misitu na ardhi ikapitishwa, na vile vile itekelezwe. |
| 31/3/2001 | Kichaka Simba (Mwaluphanga Location) | Mbunge alialikwa kwenye mchango kusaidia shule ya kichaka Simba Girls huko kwenye tarafa ya Mwaluphanga. Akiandamana na viongozi mbali mbali akiwepo makamu wa D.C. wa Kwale Bi. Musiekah, mbunge aliweza kuchangisha Kshs. 542,000/= ambako alitoa mchango wake wa Kkshs. 63,000/=. Pesa hizo ziliweza kusaidia kuongeza majengo ya shule hiyo. |
| 1/4/2001 | Ofisi | Mbunge alikutana na wananchi hapo ofisi Denyenye, ambako aliwahi kuzungumza na viongozi wa kundi la vijana la Jupiter Football Club na akawasaidia kwa Kshs. 6,000/= kujisajili kwa KFF (Mombasa). Kundi la akina mama la "Majimbooni Widows Association" yaani wale akina mama wajane wa huko Shimba Hills nao pia akawasaidia vilivyo, na pia watu wengineo mbali mbali. Siku hiyo mbunge alitumia kiasi cha Kshs. 15,000/= |
| 2/4/2001 | Lukore | Mbunge alikwenda huko tarafa ya Lukore kuhudhuria baraza aliyokuwa ameiitisha, kuzungumzia wananchi. Mambo mbali mbali ya maendeleo yalijadiliwa na vile vile mbunge akazuru shule ya upili ya Lukore ambako aliwasaidia wanafunzi kwa Kshs. 4,000/= kuweza kuenda Nakuru kwa mashindano ya uimbaji wa shule za wilaya zote za Kenya. |
| 7/4/2001 | Tiwi | Mbunge alikwenda Tiwi, kuhudhuria kwenye kundi la Halmashauri ya Shule ya Tiwi, (Board of Governors) akiwa yeye pia ni mwanachama wa kundi hilo. Majadiliano kuhusu uongozi wa shule hiyo, uhaba wa majengo yaliyopo na pia kufuzu kwa wanafunzi kwenye shule hiyo ni baadhi ya mambo yaliyopewa umuhimu. Baadaye wakati wa mchana mbunge alihudhuria hafla ya kikundi cha vijana wa mpira wa Kiweke Football Club. Hafla hiyo kusherehekea ushindi wao wa Kombe la "Kamolleh Cup Zone B" ulitokea baada ya kushinda vikundi vingine vingi. Mbunge aliwasaidia kwa ruzuku ya Kshs. 20,000/= na ngoma Kshs. 10,500/=. Hafla ilipata kiasi cha Kshs. 35,000/=. |
| 8/4/2001 | Tsimba | Mbunge alisafiri kuenda tarafa ya Tsimba, ambako aliweza kuhudhuria mchango wa kikundi cha akina mama. Huko aliwahi kukutana na akina mama hao, wananchi mbali mbali na pia viongozi kutoka sehemu hiyo. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Aliweza kuchangisha kiasi cha Kshs. 98,900/= naye akatoa mchango wake wa Kshs. 34,000/= na vile vile akalipa ngoma Kshs. 15,000/=. |
| 9/4/2001 | Lukore | Mbunge alisafiri mpaka tarafa ya Lukore ambako alihudhuria baraza huko Mkanda III ili kuzungumza na wananchi. Baraza ilihudhuriwa na watu wengi, na mbunge akawahi pia kutembelea miradi ya huko Mkanda. Mbunge alisaidia miradi ya huko kwa kiasi cha Kshs. 10,000/=. Majengo ya shule ya msingi ya Mkanda pia yatarekebishwa mwaka ujao kupatia nafasi wanafunzi kusoma vyema. |
| 22/4/2001 | Matuga | Mbunge alialikwa kuhudhuria harambee ndogo ya kuandalia harambee kubwa ili kusaidia ujenzi wa shule ya Wakunga na wasaidizi wa Hospitali (Medical Training College). Mbunge hakuweza kuhudhuria lakini aliweza kumtuma bwana Mafutu ili aweze kumuwakilisha huko. Alituma Kshs. 10,000/= kusaidia yaliyotendeka. |
| 28/4/2001 | Vuga | Mbunge alialikwa kwenda kuhudhuria harambee ya msikiti Vuga/Chirimani. Kwa sababu ya safari kwenda ulaya kwenye ziara ya kiserikali pamaja na kamati ya Ulinzi na Uhusiano wa Kimataifa. Safari hiyo iliwapeleka London- kwa Bunge la huko, Berlin (Ujerumani) na Brussels (Ubelgiji). Mbunge alituma mchango wake wa Kshs.15,000/= |
| 5/5/2001 | Ulaya | Mbunge kwenye kazi zake za bunge aliungana na kamati yote ya Usalama na Uhusiano wa Kibalozi na wakasafiri kwenda Ulaya, ili kujenga uhusiano bora na nchi za nje, na kukutana pia na wafanyi kazi wetu katika Balozi zetu za huko. |
| 12/5/2001 | Ofisi | Mbunge aliwaona wananchi katika ofisi yake huko Denyenye. Vikundi vya watu mbali mbali, Madiwani, na viongozi wa Dini walifika kujadili mambo yao kuhusu maendeleo na urekebishaji wa mambo. Mbunge aliwasaidia vikundi na watu mbali mbali kwa kiasi cha Kshs.20,000/= |
| 13/5/2001 | Burani (Mwaluphamba) | Mbunge alialikwa kusaidia mchango huko Burani kwenye shule ya Upili ya Mwaluphamba Secondary School. Watu wengi walihudhuria na mchango pia ulifana sana ambapo kiasi cha Kshs.400,000/= zilikusanywa, naye mbunge akawasaidia na Kshs. 60,000/=. Hapo hapo mbunge aliwapa watu wa huko Mwaluphamba Kshs.50,000/= ambazo zilitumwa na rafiki yake bwana Kafwihi, kusaidia madawati ya Buraini Primary School. Wakati huo huo wazee na wakulima wa Mwaluphamba walitoa malalamiko yao kuhusu ndovu waliokuwa wamevamia mashamba yao, naye mbunge akarekebisha hayo kwa kuwahimiza K.W.S. kujenga ua wa ndovu na sasa mambo ni mazuri kwa wakulima hao. |

| | | |
|---|---|---|
| 19/5/2001 | Taita | Mbunge alialikwa na rafiki yake Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais Mheshimiwa Marsden Madoka (wa Mwatate), ili akasaidie kuchangisha harambee ya kina mama. Katika mchango huo, mbunge alitoa msaada wa Kshs. 50,000/= nao mchango ukakusanya kiasi cha fedha ya Kshs. 590,000/= |
| 21/5/2001 | Nairobi | Kamati yao ya bunge ya Kibalozi, iliweza kuwakaribisha wabunge wa Urusi kutoka Russia, ambao walikuja kutembea bunge la Kenya. Mbunge na wenzake wana kamati, walikuwa na kazi kwa juma zima, wakijadiliana na wageni hao mambo mbali mbali. Pia waliwahi kuenda Mombasa na sehemu nyingine za Kenya. |
| 26/5/2001 | Mangawani | Mbunge aliwaalika waheshimiwa waziri Gideon Ndambuki na Spika mdogo wa bunge Mheshimiwa David Musila, kuja kumsaidia mchango huko Mangawani. Mchango huo ulikuwa wa kusaidia karo za wanafunzi wa shule (Bursary). Mheshimiwa Ndambuki hakuweza kuja lakini akamtuma mwenzake Mheshimiwa Musila. Nao pamoja walileta kiasi cha Kshs. 125,000/= na mbunge akatoa mchango wake wa Kshs. 75,000/=. Kwa jumla mchango ulikusanya Kshs. 360,000/= |
| 26/5/2001 | Ofisi | Mbunge alikutana na wananchi katika ofisi yake huko Denyenye ili kusikiza mambo yalio letwa na wananchi. |
| 1/6/2001 | Kwale | Mheshimiwa alihudhuria tafrija za maadhimisho ya Madaraka Day huko Kwale, ambako alihutubia umati wa watu pamoja na viongozi wengine, wakiongozwa na D.C. na hutuba zilikuwa za kusisimua. |
| 2/6/2001 | Tiwi | Mbunge alikutana na akina mama wa vikundi vya Tiwi yote huko ofisi ya Chifu wa Tiwi. Naye siku hiyo aliwakabidhi mashine za kushona nguo tatu (3), kuwasaidia kina mama hao. Sasa kina mama hao wanaweza kujimudu kufanya mambo yao wenyewe. Mashine hizo zina dhamani ya Kshs. 33,000/= |
| 3/6/2001 | Ofisi | Mbunge alikutana na wananchi huko ofisini kwake Denyenye, kwa minajili ya kusikiliza mambo yalioletwa na wananchi wa eneo la ubunge la Matuga. Mbunge alisaidia kwa Kshs. 9,500/= |
| 16-17/6/2001 | Ofisi | Mbunge alitumia siku mbili zote hizi kukutana na wananchi ambao walikuja kwa wingi kutoka kila pembe ya eneo lake. Vikundi mbali mbali, wananchi, viongozi na vijana walimtembelea mbunge kujadili mambo yao. |
| 23/6/2001 | Tiwi | Mbunge alihudhuria mkutano wa halmashauri ya Shule ya Upili ya Tiwi (BOG) ili kujadili mambo ya uendeshaji wa shule hiyo. Usimamizi wa shule hiyo, kama vile walimu, majengo, madawati, na mengineyo. Wanachama wapya wa halmashauri hiyo pia walichaguliwa. |
| 25/6/2001 | Tiwi | Mbunge alihudhuria mkutano wa baraza huko Tiwi, akiandamana na D.C. wa Kwale. Mada za kuhusu mashamba, barabara na shule yaligusiwa. Hata mambo ya usalama wa sehemu hiyo yalipewa umuhimu wake na kupangwa upya. |

| | | |
|---|---|---|
| 7/7/2001 | Waa | Mbunge alikwenda tarafa ya Waa kujumuika na vijana wa mpira wa Zimbabwe. Walitoa mwaliko kwa mbunge wao aende katika sherehe zao za kikombe cha mpira. Mchango wao katika tafrija hizo ulipata fedha kiasi cha Sh. 60,000/= naye mbunge akawapa msaada wa Kshs. 20,000/= pamoja na ngoma Kshs. 10,000/=. |
| 8/7/2001 | Ofisi | Mbunge alikutana na wananchi huko ofisini Denyenye, na baadaye alienda kuonana na vijana na akina mama huko Pungu. Vijana na akina mama hao walitaka kumuona ili waweze kumweleza mambo na matatizo fulani yaliyo wakumba. Mbunge aliwasaidia kwa Kshs. 15,000/= |
| 14/7/2001 | Ng'ombeni | Kwa mara nyingine tena mbunge alifika katika shule ya msingi ya Ng'ombeni kuhudhuria sherehe za kufuzu kwa mitihani ya darasa la nane (8) kwa sehemu ya "Ng'ombeni, Tiwi, Waa Zone". Shule hiyo ya Ng'ombeni kwa mara ya pili ilikuwa ya kwanza kwenye sehemu hiyo na kwa hivyo sherehe zikafanywa hapo kwao. Zawadi kwa walimu na wanafunzi zilipeanwa. Na kisha mbunge akawapa kiasi cha Kshs. 30,000/= kununua madawati ya kusomea ili waweze kusoma vyema. Ahadi ile ya tarehe 3/4/2000 na tarehe 15/5/2000 ilikaririwa tena na mbunge naye akasema shule yoyote ile katika sehemu yake ya ubunge itakayo kuwa ya kwanza wilayani Kwale yeye ataipatia Kshs. 200,000/= na ile itakayo kuwa ya kwanza kwenye sehemu ya Pwani (Ngombeni, Waa, Tiwi Zone) yeye ataipatia Kshs. 25,000/=, au Zone yoyote ile kwenye eneo lake la ubunge. |
| 15/7/2001 | Waa | Mbunge alikwenda Waa kusaidia kufanya mchango kwa vijana wa tarafa hiyo- "Waa Youth Groups." Harambee haikuhudhuriwa na watu wengi na hivyo pesa zilizo changwa zilikuwa kidogo. Mchango wote ulikuwa Kshs. 155,000/= ,naye mbunge akatoa Kshs. 33,000/= pamoja na ngoma Kshs. 10,000/=. |
| 22/7/2001 | Majimboni | Mheshimiwa aliandamana na waziri mdogo katika wizara ya serikali za wilaya Mhe. Mohammed Salim Fumo, kwenda Majimboni. Huko walisaidia kuchangishwa kwa Bursary Fund.<br>Mgeni wa heshima waziri Madoka hakuweza kufika lakini alimtuma msaidizi wa waziri huyo kuja kumwakilisha. Waziri alileta Kshs. 80,000/=, naye waziri mdogo akasindikiza na Kshs. 20,000/= na mbunge akatoa Kshs. 75,000/= na akalipa ngoma Kshs. 15,000/= na viburudisho Kshs. 10,000/=. Kwa jumla mbunge alitoa Kshs. 100,000/= kwa mambo hayo. Mchango huo ulikusanya Kshs. 429,000/=. |
| 23/7/2001 | Amerika | Mbunge aliondoka Kenya kwenda Amerika kwa mwaliko wa serikali ya huko. Mbunge alitembelea taasisi mbali mbali na akajionea jinsi serikali ya huko imeweza kujihami na ufisadi wa kiuchumi (Corruption). |

| | | |
|---|---|---|
| 28/7/2001 | Ng'ombeni | Wakati bado yuko safarini Amerika, mwaliko wake wa kuchangia Ng'ombeni Secondary School uliendelea. Naye mbunge aliwakilishwa na bwana Mafutu aliyesaidia kuchangisha kiasi cha Kshs. 890,000/= ambapo alitoa mchango wake wa Kshs. 60,000/=. Mchango huo ulikuwa wa kusaidia jengo la maktaba (Library) kwa shule hiyo. |
| 4/8/2001 | Mwingi | Kwa mwaliko wa mbunge mwenzake Mhe. David Musila kusaidia katika mchango wa shule ya wasichana, mbunge alituma mchango wake kupitia Mhe. Elijah Sumbeiwo wa kiasi cha Kshs. 25,000/= katika mchango huo. |
| 13/8/2001 | Nairobi | Mbunge alirudi Nairobi kutoka safari yake huko Amerika, akiwa na mambo mengi yaliyojadiliwa na kupitishwa kati ya serikali hizo mbili. |
| 18/8/2001 | Waa | Mbunge aliwaalika wabunge wengine, waheshimiwa Simeon Nyachae, Jimmy Angwenyi, Henry Obwocha, Zebedeo Opore, James Magara na Karisa Maitha kuja kusaidia mchango wa vikundi vya akina mama wa Waa. Mchango huo ulikusanya pesa kiasi cha Kshs. 573,000/=. Mbunge naye akatoa mchango wa Kshs. 95,000/= na akalipa ngoma Kshs. 8,000/= na misindikizo ya Kshs. 5,000/= (i.e Kshs. 108,000/=). Wabunge wenzake nao wakamletea Kshs. 10,000/= kila mmoja (yaani Kshs. 50,000/=). |
| 19/8/2001 | Kizibe (Mwaluphamba) | Baada ya hapo mbunge hakuchoka, aliendа Kizibe – tarafa ya Mwaluphamba na akasaidia kuchangisha kwa shule ya msingi kiasi cha Kshs. 110,000/= naye akasaidia kwa Kshs. 30,000/= |
| 25/8/2001 | Ofisi | Mbunge alikutana na wananchi huko ofisi ya Denyenye kama kawaida yake. Kisha alienda Kaloleni kuhudhuria harusi ya mtoto wa rafiki yake bwana Kafwihi huko Kilifi. |
| 26/8/2001 | Tiwi | Mbunge alifika Tiwi Chai kuhudhuria mchango kwa msikiti wa " Annas Bin Malik" ambako alisaidia kuchangisha kiasi cha Kshs. 150,000/= naye akachanga zake Kshs. 30,000/=. |
| 8/9/2001 | Mwaluphanga | Mbunge alisafiri mpaka Mwaluphanga Shimba Hills, kusaidia mchango wa Kichaka Simba Parish ya Catholic Church. Huko alikusanya kiasi cha Kshs. 29,000/= naye akatoa mchango wake na Kshs. 10,000/=. |
| 9/9/2001 | Ofisi | Mbunge alikutana na wananchi huko ofisini Denyenye. Watu walikuwa wengi na matatizo yao. Vikundi navyo vikaja na mijadala mbali mbali naye mbunge aliwahi kusaidia kwa kiasi cha Kshs. 25,000/=. |
